

"Usisite kujifunza ! Kwa njia hiyo tutaweza kuushinda ujinga..." (mwanafunzi mmoja)

Kuanzia mwezi wa saba hadi mwezi wa kumi na moja mwaka 2016, takribani watu 20 walijiunga na darasa ili kujifunza kusoma na kuandika. Sehemu ya kujifunzia ilikuwa ni katikati ya soko la samaki katika chumba cha mikutano cha bodi ya utawala. Tunawashukuru kwa msaada wao. Tulikuwa tunajifunza mara tatu kwa wiki na walimu wawili kutoka wilaya ya llala walikuwa wanakuwa kutoa mafunzo. Walitumia mbinu mpya inaoiyitwa: "Ndiyo Ninaweza" iliozoleka kuwafundisha watu wazima.

Kundi hilo la wanafunzi lilijumuisha watu wazima na vijana ambao hawakupata nafasi ya kusoma hata shule ya msingi. walikubali kuja kama vile mtoto aliye tayari kujifunza na kuacha kujisikia aibu kama watu wengine, walionyesha nguvu na ujasiri. Darasa lilifanyika karibu na mazingira wanayoishi na kufanya kazi, hii ilionyesha kwamba kwa kupata mazingira mazuri ya kujifunzia watu wanaweza kufanikiwa katika hali yeoye ya maisha.

Wanafunzi walisema hamasa ya kwanza ya wao kujifunza ilikuwa ni kuboresha maisha na kupata ajira nzuri. Mwishoni ni swala la kuheshimika na kuwa mtu kama wengine. Ninaweza kujua haki zangu vizuri. Jinsi walivyoishi pamoja ilikuwa ni zaidi ya darasa, hakika waliisha kwa namna ya kufanana ambapo walijifunza kufahamiana zaidi. Walifurahia kukutana pamoja kila juma, wengine wakijianda na kushiriki kikamilifu kuanda kipindi darasani kwa kupanga viti, kuanda mafaili na ubao.

Mmoja wa wanafunzi alisema: Tunajiskia kama familia, tunakutana na kubadilishana mawazo na kuwasaidia majirani wengine. Tunasaidiana, tuko makini ili mtu yeoye asipotee.

Wahitimu wa darasa la Watu Wazima la kujua Kusoma na Kuandika la ATD mwaka 2016 !

Tamko la Jenifa kwa niaba ya wanafunzi wote, wakati wakushereke Siku ya kuutokomeza ya umaskini uliokithiri :

"Wakati nilipokuwa mdogo sikupata nafasi ya kwenda shule, maisha yalikuwa magumu. Nilipoamua kuijunga na darasa, Changamoto moja iliyonikabilii ni jinsi watu walionizunguka walivyonitazama, maneno yao-walinicheka, walinitania nilivyoenda darasani, kuiacha kazi yangu. Lakini nilikuwa ninajua ninachokifanya. Nilifurahi sana kuwa sehemu ya kikundi, Naona nahitaji kuweka jitihada kubwa ili nifanye vizuri. Tunasaidiana, tuko makini ili mtu yeoye asipotee. Na mimi pia ninapata msaada kutoka kwa wanangu japo pale mwanzo walikuwa wakinicheka. Sasa wanajivunia mimi kwasababu sasa ninajua kusoma na kuandika. Sasa tunapata muda wa kusoma pamoja.

Leo ninaweza kurnunua kwa bei nzuri, ninaweaza kusoma kifungashio, ninaweza kubadilisha, kuhesabu fedha zangu, sipotezi tena fedha kwenye biashara yangu ndogo. Inanifurahisha, ninajiskia vizuri zaidi kwenye maisha yangu kwa ujumla - kwa sababu kabla nilijihisi kama mlemau, ilikuwa ngumu kuwasiliana, nilikuwa nakaa tu kimya.

Sikudhani kama ningeweza kupata nafasi hii siku moja - nafikiri kwa wote sisi tulioiosa fursa ya kwenda shule, ninawaasa kama wakisikia kuna fursa wasisite kwenda kujifunza - kwa njia hiyo tutatokomeza ujingga."



Kundi la wanafunzi wa Soko la Samaki wakiwa pamoja na waalimu wao na Maafisa Elimu wa Wilaya ya llala

Mwanafunzi mmoja
"Leo naweza kusoma gazeti, leo naweza kubadilishana mawazo na wenzungu juu ya kinachoendelea duniani, sasa najihisi kabisa kama sehemu ya jumua na nimeachana na hali ya kutengwa. Aibu imekwisha najihisi imara kabisa."

Jiunge nasi!

- Unaweza kuwa mfuasi wetu na kutuunga mkono kupitia Facebook yetu:
<https://www.facebook.com/atd.duniayanne>
- Kuona makala kuhusu Elimu Kwa Hatua zote, angalia kwenye tovuti ya ATD Dunia ya Nne:
www.atd-fourthworld.org

Wasiliana nasi!**JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA**

December 2016



"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika".
- Joseph Wresinski (1917-1988) founder of ATD Fourth World -

Tahariri

Wependwa marafiki,

Tunapomaliza mwaka 2016 hebu tuzamishe nafsi zetu katika tafakari ya kauli zifuatazo:
"Umaskini haukuletwa na Mungu, bali unasababishwa na binadamu kwa sababu walionacho hawagawani na wasionacho".

Hii kauli ya mama Theresa wa Kalkuta. "Umaskini uliokithiri ni kazi ya wanadamu na ni wanadamu pekee wanaoweza kuutokomeza". Kauli ya Joseph Wresinski muasisi wa ATD. Uchoyo, ubinasi, kujilimbikizia mali na mengine ya namna hiyo yamekuwa chanzo cha vita, vurugu, uharibifu wa mazingira na zaidi janga la umaskini ambalo ni uvunjifu wa haki za binadamu.

Sisi wana ATD tukishirikiana na wadau wengine ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba hawa wanarejeshewa utu na heshima yao na hivyo kwamba waweze kusimama na kusonga mbele kuleta maendeleo yao binafsi na katika jamii. Umoja wetu, ushiriki wetu na kujitoa kwetu sisi ni muhimu kwa sababu sisi tunabaki kuwepo wakati wana timu hubadilika kila baada ya muda. Ni jukumu letu kujenga jamii inayojiamini na ilio tayari kushiriki kuleta maendeleo binafsi na ya jamii kwa ujumla.

Mwaka huu wa 2016 umekuwa wa mafanikio kwetu sote kama shirika. Tumeshiriki katika shughuri mbalimbali na tafiti na hivyo kujenga mahusiano zaidi. Hii imejiakisi katika maadhimisho ya Oktoba 17 ambayo yalifana kote, Dar, Njombe na Dodoma. Washirika walitoka katika nyanja mbalimbali, wanataluma, wawakilishi kutoka serikalini na mashirika mbalimbali. Kimataifa tumeshiriki katika mukutano wa Bangui Afrika ya Kati, na tunataraja kushiriki katika mukutano wa Dakar kule Senegal. Yote hii ni katika maadhimisho muhimu ya mwaka 2017: miaka 100 ya kuzaliwa Wresinski, miaka 60 ya kuanzishwa shirika, miaka 30 ya kuadhimisha Oktoba 17. Yote haya ni wajibu wetu na tunapaswa kujitoa kwa dhati.

Niwatakie Krismasi njema na Heri ya mwaka mpya.

Aslaam Aleykum,

Constantine S. Munema.



Mama Kaijage (Chasimba) akitoa ushuhuda kuhusu jinsi ilivyo vigumu kwa familia kupata cheti cha kuzaliwa.
Octoba 15, Makembusho, Dar es Salaam

Mwaka ujao itakuwa sherehe muhimu ya miaka 30 ya Siku ya Kimataifa ya kuutokomeza umaskini uliokithiri. Mwaka huu maadhimisho ya tarehe 15 Oktoba ilikusanya maelfu ya watu pamoja. Kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa ni ushirikishwaji wa watu wote ili kuutokomeza umaskini wa kila aina, kuhakikisha watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri ndio washirika wa kwanza katika kila jumbo, maamuzi na miradi.

Mwaka huu, kamati ya Oktoba 17 inataka kutoa taarifa kwa wajumbe wa ATD, familia na marafiki ambao mara nyingi walisema, "Kwa kweli, hatujui haswa taasisi inafanya nini katika nchi kwa kipindi cha mwaka mzima". Dar es Salaam, katika kijiji cha Makembusho, familia kutoka maeneo mbalimbali, marafiki, maafisa elimu na wanaharakati wa kudumu wa kujitolea walitoa shuhuda, changamoto na mafanikio kwa yale yanayoendeshwa na taasisi hapaTanzania.

Kwa kila hatua shuhuda zililenga suala zima la ushirikishwaji kwa wale wote ambao wahakuweza kusiskika na kuwawezesha kushiriki. Aidha kwa vitendo, kuamua na kuwaita watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri au kwa baadhi ya miradi ni inayozinduliwa kwa kushirikiana na taasisi na kutoptana na hivyo taasisi inawapa mstari wa mbele wale wote waliokuwa na uzoefu wa maisha ya kutengwa kuwa waathirika wa kwanza.

Mradi wa yeti vyta kuzaliwa (1): Mama Kaijage, apata cheti cha kuzaliwa kwa kila mtu ni haki ya kutambulika ambayo inaruhusu kila mtu kuwa sehemu ya jamii. umuhimu ni jinsi gani ya kuhusisha watu, hasa wale ambao wameshaulika kufahamu namna ya kufanya kazi na ngazi za utawala, namna watu ambao wamepata uzoefu huu wanaweza kuwapatia wengine, kubadilishana maarifa na kusaidiana. Kila mmoja atakuwa na jukumu la kufanya.

(1) Umedhaminiwa na Hilfe for Africa and AFD



Kamba ya Mshikamano na washiriki
Siku ya Kutokomeza umaskini uliokithiri 2016, Dar es Salaam



Uhamasishaji wa marafiki
Siku ya Kutokomeza umaskini uliokithiri
- Njombe and Dodoma -

Elimu kwa Wote (2): timu iliowasilisha mradi wa utafiti wa Elimu Kwa Wote (tazama jarida la Agosti 2016) hii Oktoba 15 hapa Dar es Salaam ilisisitizwa juu ya nguvu ya kundi linalojumuisha watu wanaotoka katika maeneo yalijotengwa, walimu na wanaharakati wa kudumu wa kujitolea wa ATD. Utafiti wote ulisimamiwa na kundi hili, kuanzia upangaji, mahojiano, kwa kazi ya uchambuzi na kuandika mapendekezo. Watu wanaoishi katika umaskini wanaweza kuleta ujuzi wao na kuhakikisha hitimisho thabiti kwa kuzingatia hali halisi na hofu ya wazazi na watoto ili kuhakikisha kuwa wanaweza kupata elimu ya msingi.

Darasa la kufuta ujinga (3): Watu kutoka Magogoni Soko la Samaki walikuwa wakidai kuanzishwa kwa darasa la kufuta ujinga. Kupitia ushiriki wa marafiki wa taasisi wanaofanya kazi pale, darasa lilitangazwa na kufunguliwa na watu wapatao ishirini. Kundi la wanafunzi walihudhuria sherehe ya Oktoba 15 na walimu na mwakilishi wa wilaya ya Ilala kutoka Idara ya Elimu. Baada ya darasa, wanafunzi, walisema kusoma na kuandika ni hatua ya kuwa sehemu ya jamii na kuwa hai katika mradi wowote (angalia ukurasa wa mwisho).

Kubaini vipimo vya umaskini na jinsi ya kuvipima (4): Je, mradi wa utafiti wa kuelewa umskini ni nini, vipimo vyake na jinsi ya kuvipima. Ni fursa ya kushirikisha watu wanaoishi katika umaskini na kufikiri upya pamoja nao kuhusu umaskini ni nini na jinsi ya kuutambua pamoja na washiriki wengine kama vile wasomi, watunga sera au wafanyakazi wa jamii. Njia ya kuunganisha Maarifa itatumika kwa watu wanaokibiliwa na umaskini uliokithiri na kutengwa na jamii watawezeshwili ili kubadilishana mawazo na washiriki wengine na kutambulika kama watafiti wenza, kwa usawa (soma kuhusu uzoefu wa Gabriel).

(2) Umedhaminiwa na UNESCO na AFD
(3) Umedhaminiwa na Hilfe Afrika na AFD
(4) Umedhaminiwa na AFD

Ndugu Gabriel Chacha ni mwanasayansi jamii, mwenye uzoefu wa kazi wa muda mrefu katika mashirika ya kimataifa na yasiyo ya kimataifa yanayoishughulisha na kazi za kijamii na uchumi. Pia ameshiriki katika kazi mbalimbali za utafiti. Alijunga na timu ya utafiti ya ATD Dunia ya Nne itakayo fanya utafiti kujua maana ya umaskini uliokithiri pamoja na kubaini vipimo vyake. Njia itakayotumiwa na ATD Dunia ya Nne kufanya utafiti huu, amempa mbinu mpya ya kufikiri na kutoa kipaumbele katika maarifa walijonayo watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri pamoja na kuwashirikisha. Timu yake ilutambulisha mradi huu wakati wa siku ya kutokomeza umaskini uliokithiri Duniani iliyoadhimishwa Dar es Salaam, alitueleza inamaanisha nini kwakwe.

Tofauti kubwa ipi ukilinganisha na kazi ulizokwisha fanya?

Kilicho nivutia ni utamaduni wa dhati uliopo wa kuheshimu utu na haki za binadamu, hasa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Hapa hatufanyi kazi kwa ajili ya isipokuwa tunafanya **pamoja na** watu kwa njia ya mshikamano na ushirikishwaji. Huko nilikokuwa nikifanya kazi hali haikuwa hivyo. Mashirika yamekuwa yakiwasikiliza, kufanya uchunguzi na mwisho kutoa majibu kulingana na fikra zao, ni mabadiliko gani tunapaswa kufanya ili kutokomeza maisha yenye dhiki. Lakini hapa ATD Dunia ya Nne, kilakitu huanza kutokana na uzoefu, mchangano wa watu walio katika maisha ya kutengwa siku zote.

Ni changamoto ipi kubwa ninayoiona?

Changamoto iliyopo ni kuwezesha uwakilishi ulio sawa na wa haki Baada ya wiki chache nimeelewa zaidi kwamba ushirikishwaji sio tu kuwasikiliza watu isipokuwa ni kuwashirikisha katika hatua zote kuanzia mwanzo hadi mwisho- kuandaa, kupanga, kutekeleza, kuchambua na kufikia majumuisho. Nina matumaini kupata kitu muhimu saana, kitu kipyaa kabisa zaidi ya yale tulijofunza. Kitabdalisha kabisa utaratibu uliozooleka kwenye taasisi na itawasaidia watu wanaotoa maamuzi kutoa maamuzi yanayozingatia hali halisi ya maisha ya watu.

Tulianda tukio katika eneo la kikundi cha Smith Kisangani Group katika Mkoa wa **Njombe**, tulitoa ujumbe kuhusu atd kwa marafiki na kuwafahamisha kuhusu siku hii ya kimataifa ya kutokomeza umaskini.

Marafiki toka maeneo mbalimbali walihudhuria Kutoka Mbeya, sehemu nyngine kikundi cha ufundi toka katika Wilaya ya Makambako, Ludewa kikundi cha kilimo cha maparachichi, wakulima wa mboga mbogamboga, wanahabari walishiriki na walirusha habari katika Radio, kundi la walini, kiwanda cha maziwa na rafiki raia wa Ujerumani. Zaidi ya watu 60 walihudhuria maadhisho ya 17 Oktoba mwaka huu.

Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa kufanya kazi pamoja katika mshikamano ili kuondoa umaskini.

Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa kushikamana kwa pamoja kupambana na umaskini.

Washiriki walivutiwa na walifarjika na unyonge uliwatoka na waliona tukiwa pamoja tunaweza kusonga mbele. Tatizo la umaskini si pesa tu, pia kutoshirikishwa kimawazo kunakosababisha kutojifunza kutoka kwa wengine. Tunatakiwa watu tuwe pamoja katika kila jambo watu wa hali ya juu na watu wa hali ya chini ili ipatikane fursa ya kujifunza kutoka kwa wengine

Njombe, Roeuben Mtiti

Ujumbe wa siku ulikuwa kutokomeza ujinga hebu tuwapeleke watoto wetu shule.

Tulienda kijiji cha jirani **Mbabara B** tuliadhimisha siku ya tarehe 17 Oktoba na kuhusu kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa ili kutokomeza umaskini, ujingga tupeleke watoto wetu shule. tulipata marafiki wapya na walivutiwa na maadhisho. Maadhisho yalijumuisha vijiji vitatu Bihawana Mbabara (B) ambako maadhisho yalisanyikia kijiji cha Khome jumla ya watu 44 walishiriki katika maadhisho hayo. Washiriki walisisitiza suala la mshikamano kushirikishana na kushikamana katika umoja.

Zaidi ya yalipangwa na kufanya 260 matukio ilipangwa katika nchi 54 katika mwaka 2016